

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Anuani ya Simu: "TAMISEMI"
Simu Na: (026) 2322848, 2321607
2322853, 2322420
Nukushi: (026) 2322116,
2322146,2321013
Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz



Tawala za Mikoa na
Serikali za Mitaa,
S.L.P. 1923,
DODOMA.

28 Agosti, 2018.

TAARIFA KWA UMMA

Yah: KUSITISHWA KWA MUDA KWA ZOEZI LA UHAMISHO

Itakumbukwa kwamba katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) imefanya uhamisho kwa baadhi ya watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa .

Baada ya kufanyika kwa uhamisho huo imeonekana kuwa ipo haja ya kufanya tathmini ya kina juu ya namna zoezi la uhamisho linavyofanyika ili kuweza kuboresha zaidi utoaji wa huduma hiyo. Sambamba na tathmini hiyo, Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora zipo katika hatua za kutengeneza mfumo wa kieletroniki wa maombi ya uhamisho ili kuwawezesha watumishi waliopo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kupata huduma za uhamisho kwa haraka na urahisi zaidi.

Kwa mantiki hiyo, tunapenda kuwataarifu watumishi wote waliopo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa zoezi la uhamisho wa Watumishi kutoka katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa limesitishwa kwa muda hadi hapo tathmini ya kina ya utoaji wa huduma hiyo itakapokamilika.

Baada ya zoezi la tathmini kukamilika, mtajulishwa kuendelea kwa zoezi hili kupitia tovuti rasmi ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI na mitandao yake ya kijamii ambayo ni. (www.tamisemi.go.tz)

Imetolewa na:



Rebecca Kwandu

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,

Ofisi ya Rais,

Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

27 Agosti, 2018.